

Maswali

1. Watu wa Kanaani waliabudu nini?
2. Abramam na familia yake waliabudu nani?
3. Mbona Abramam na familia yake walisafiri wakizunguka nchi?
4. Mbona watumishi wa Abramam na watumishi wa Lutu waligombana?
5. Abramam alisema eti wafanye kitu gani ili wagomeshe ugomvi?
6. Mbona Abramam aliacha Lutu achague kwanza?
7. Lutu alichagua upande gani wa nchi?
8. Abramam alikuwa na nchi ya namna gani?
9. Mungu alifurahia Abramam. Mungu aliahidi Abramam nini?
10. Nani alilinda Abramam na familia yake?

Majibu

1. Watu wa Kanaani waliabudu sanamu.
2. Abramam na familia yake waliabudu Mungu.
3. Walisafiri wakizunguka wakitafuta nyasi na maji ya kondoo na mbuzi wao.
4. Waligombana kwa sababu hakukuwa na nyasi na maji ya kuwatosha.
5. Abramam alisema kwamba yeye na Lutu watengane na wakae tofauti.
6. Abramam alikuwa mzuri na mkarimu. Aliamini kwamba Mungu atalinda popote atakapokuwa.
7. Lutu alichagua eneo nzuri yenye ilikuwa na nyasi nyingi na maji mengi.
8. Eneo lenye Abramam alikaa ilikuwa kavu na nyasi kidogo.
9. Mungu aliahidi kumpa Abramam na watoto wake nchi yote milele.
10. Mungu alilinda Abramam na familia yake

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



4 Abramam na Lutu

Marejeo

Mwanzo 13:5 – 18

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Abramam alibarikiwa kwa sababu aliamini Mungu. Lutu alichagua njia rahisi na hakuonyesha imani kwa Mungu.

Maneno maalum

- 4.1 Kanaani + watu waliabudu sanamu + Abramam aliabudu Mungu + mahema + tenga
- 4.2 Abramam + Lutu + kondoo wengi + hakuna nyasi ya kutosha + ugomvi
- 4.3 Abramam + msigombane + ishi mbali mbali + Abramam aliamini Mungu + Lutu alichagua kwanza
- 4.4 Lutu alichagua eneo nzuri + Lutu alifurahi + nyasi nyingi na maji
- 4.5 Mungu alifurahi + Abramam aliamini + nchi yote milele + Mungu alilinda Abramam

4.1 Abramam, Sarai na Lutu walitii Mungu na wakaenda kuishi kwa nchi ya Kanaani. (Hiyo nchi inaitwa Israeli sasa). Watu walioishi kwa nchi ya Kanaani hawakupenda Mungu. Waliabudu sanamu.



Abramu na familia yake waliabudu Mungu. Abramam, Sarai na Lutu waliishi kwa mahema. Walijitenga na watu wa hiyo nchi. Walisafiri wakizunguka wakitafuta kondoo na mbuzi wao nyasi na maji.

4.2 Wote Abramam na Lutu walikuwa na kondoo na mbuzi wengi.

Walihitaji nyasi nyingi na maji ili itoshe kuwalisha wote. Wakati wa jua kulikuwa na joto na kulikauka sana. Vijito vilipokauka, maji yalichotwa kwa vizima na hiyo ilikuwa kazi ngumu mno. Iliwachukua muda mrefu kuzunguka na kutafuta malisho ya mifugo wengi. Wakati nyasi na maji haikupatikana ya kuwatosha, watumishi wa Abramam na Lutu waligombana wenyewe kwa wenyewe.

4.3 Abramam alipoona huo ugomvi, hakufurahia. Alijua kwamba Mungu hakutaka watu wagombane. Aliambia Lutu, "Haitakiwi kuwe na ugomvi kati ya watumishi wangu na watumishi wako kwa sababu sisi ni familia moja. Hebu tutengane. Wewe chagua mtaenda upande gani na mimi na watumishi wangu tutaenda upande mwingine. Halafu sisi wote tutakuwa na nyasi na maji ya kutosha."

Abramu alikuwa mjomba wa Lutu. Alikuwa ndiye mkubwa. Ndiye angekuwa mtu wa kwanza kuchagua upande wa kuenda. Abramam alikuwa mzuri tena mkarimu kwa hivyo aliaacha Lutu achague kwanza. Abramam aliamini kwamba Mungu atamlinda popote atakapoishi

4.4 Abramam na Lutu walienda juu ya mlima. Kule juu wangeona nchi yote ya kule. Lutu aliangalia akaona upande moja wa nchi ulikuwa kijani kibichi na maji mengi hata na nyasi ya kondoo. Lakini pande zingine zote zilikuwa kavu na nyasi zilikuwa chache. Lutu alijichagua upande mzuri zaidi. Kwa hivyo Lutu na Abramam walijitenga na kwenda kuishi kwa nchi tofauti.

Lutu alifurahi sana kwa sababu alichagua pahali pazuri pa kuishi. Alifurahi kwa sababu alikuwa na maji mengi na nyasi nyingi ya kutosha kondoo wake na mbuzi. Lakini Abramam naye alifurahi. Alijua kwamba Mungu atamshugulikia.

4.5 Abramam alisimama juu ya kilima. Mungu alifurahia kwa sababu Abramam alikuwa mzuri tena mkarimu. Alifurahi kwamba Abramam alimwamini. Mungu alimwambia Abramam angalie mzunguko wa nchi yote akiwa kule kilimani. Mungu alimwambia Abramam, " Nchi **yote** yenye unaangalia nitakupa wewe na watoto wako wote milele. Nitafanya taifa kubwa kutoka kwako. Enda utembe kwa nchi yote kwa kuwa nitakupa wewe." Mungu alilinda Abramam na kumshugulikia yeye na familia yake.